#MAKINIKIA Kutoka Kwa Jim Rhon Na Falsafa Yake Ya Maisha Ya Mafanikio.

Rafiki yangu mpendwa,

Ni nani asiyependa kuwa na maisha ya mafanikio?

Kwa hakika hakuna asiyependa kuwa na mafanikio kwenye maisha yake.

Lakini sasa, mbona ni watu wachache sana ambao wamefanikiwa?

Kwa nini wengi wanaendelea kuwa na maisha duni licha ya kupatikana kwa fursa nyingi kwa kila mtu?

Jibu anatupa aliyekuwa mwandishi na mhamasishaji Jim Rhon ambaye akiwa na miaka 25 alikuwa amefulia kabisa (broke) lakini akiwa na miaka 31 alikuwa milionea.

Je ni kitu gani kiliweza kumtoa kwenye kufulia mpaka kuwa milionea ndani ya miaka 6 pekee?

Jim Rhon anatushirikisha kwenye kijitabu chake kidogo kinachoitwa MY PHILOSOPHY FOR SUCCESSFUL LIVING.

Jim anasema, kutengeneza falsafa yake ya maisha ya mafanikio ndiyo kulimwezesha kupiga hatua hiyo kubwa na kuendelea kuwa na maisha ya mafanikio.

Yafuatayo ni mambo muhimu tunayoweza kujifunza na kuyafanyia kazi kwenye maisha yetu ili na sisi tuweze kufanikiwa pia.

1. Manunuzi muhimu sana unayofanya kwenye maisha yako siyo kwa kutumia fedha, bali kwa kutumia muda. Unapoweka muda wako kunakugharimu sana. Wekeza muda wako kwa umakini, ukishaupoteza hauwezi kurudi tena.
2. Muda ukishapotea haurudi, kuwa bahili sana wa muda wako.
3. Uwekezaji bora kabisa unaoweza kufanya kwenye maisha yako, matumizi sahihi ya muda wako ambayo yatakuwa na manufaa kwako ni kujifunza. Unapojifunza kwa kusoma vitabu au kuhudhuria semina, unapata hazina ambayo haitapotea kamwe.
4. Unapojifunza, unapata mawazo mbalimbali, na katika mawazo hayo, moja linaweza kuleta mabadiliko makubwa sana kwenye maisha yako. Hivyo usijiwekee ukomo kwenye kujifunza, hujui wazo la mabadiliko utalipata wapi na wakati gani.

5. Kila binadamu ana uwezo mkubwa wa kufanya mabadiliko kwenye maisha yake. Kama ambavyo kiwavi anaweza kubadilika na kuwa kipepeo, ndivyo na sisi tunaweza kubadilika kutoka pale tulipo sasa na kufika mbali zaidi.
6. Msingi mkuu ambao Jim Rhon anasema ulimpa mabadiliko makubwa ndani ya miaka 6 ni huu; Unalipwa kulingana na thamani unayotoa sokoni, hivyo kama unataka kulipwa zaidi, toa thamani zaidi.
7. Lakini pia unalipwa kulingana na thamani yako binafsi, hivyo kama unataka kulipwa zaidi, basi kuza zaidi thamani yako binafsi. Unakuza thamani yako kwa kuwa bora zaidi kila siku, kupitia kujifunza na kufanya mabadiliko kwenye maisha yako.
8. Elimu ya maendeleo binafsi (personal development) ndiyo elimu pekee itakayokufikisha kwenye mafanikio makubwa. Jim Rhon anasema, elimu ya darasani itakupa kazi lakini elimu binafsi itakupa utajiri. Wekeza kwenye elimu ya maendeleo binafsi kwa kujifunza kila siku na hutabaki pale ulipo sasa.
9. Unapotaka kufanya mabadiliko makubwa kwenye maisha yako unapaswa kuwa na menta, mtu ambaye atakuongoza kwa usahihi kupiga hatua kubwa. Peke yako ni rahisi kuishia njiani, lakini unapokuwa na menta anahakikisha unapiga hatua.
10. Menta anakusaidia kuondokana na fikra hasi zinazokuzuia kupiga hatua. Kila mmoja wetu ana hofu, fikra na mitazamo ambayo inamzuia kupiga hatua. Peke yako huwezi kuzitambua, lakini menta wako ataona kwa urahisi na kukusaidia kuondokana nazo.
11. Kikwazo kikubwa kwa mafanikio yako ni wewe mwenyewe. Siyo hali ya uchumi, kazi au biashara na wala siyo mazingira au hali ya hewa. Kikwazo kikubwa ni wewe mwenyewe, ukiweza kuvuka kikwazo hicho, hakuna kitakachokuzuia. Jim Rhon anakuambia uandike sababu zote unazojipa kama kikwazo kwako kufanikiwa kisha choma kabisa karatasi hiyo na utabaki na uhuru wa kupiga hatua.
12. Msingi wa falsafa ya maisha ya mafanikio ni huu; kama utaweka juhudi kubwa kwenye kazi yako utapata kipato cha kuendesha maisha, kama utaweka juhudi kubwa kwako binafsi, utatengeneza utajiri. Hivyo unapaswa kuweka juhudi kubwa kwako binafsi, kwa kujiboresha zaidi ili uweze kufanikiwa sana.
13. Mafanikio hayatafutwi, bali mafanikio yanavutwa. Huwezi kuyatafuta mafanikio ukayapata, bali unaweza kuyavutia mafanikio kwako kwa

wewe kuwa mtu bora. Ndiyo maana ni muhimu kuweka juhudi kwako binafsi na kuwa bora zaidi.

14. Kupata utajiri na mafanikio kunaweza kuwekwa kwenye kitu kimoja, kuwasaidia wengine. Utafanikiwa kwa kiwango ambacho unawasaidia wengine. Usijiulize wengine wanakupa nini ili ufanikiwe, bali jiulize unawapa wengine nini ili ufanikiwe.
15. Kusudi lako kuu kwenye maisha linapaswa kuwa kuwasaidia wengine. Jiulize kazi unayoifanya inawasaidiaje wengine, inafanyaje maisha yao kuwa bora zaidi. Kadhalika kwenye biashara yako. Kadiri unavyotatua matatizo makubwa na yanayowasumbua wengi, ndivyo unavyofanikiwa zaidi.
16. Ili kusalimika kwenye zama hizi za ushindani mkali, unahitaji kuwa na fani zaidi ya moja. Zile zama za kuwa na fani moja na kubobea kwenye fani hiyo zimepitwa na wakati. Mambo yanabadilika kwa kasi na ushindani ni mkali. Chagua kuwa na fani zaidi ya moja, ambazo ukizifanyia kazi kwa pamoja utakuwa mtu wa tofauti ambaye hana ushindani.
17. Tofauti ya masikini na matajiri inaanzia kwenye falsafa wanazoishi. Falsafa ya masikini ni hii; tumia kwanza fedha zako, halafu kiasi kinachobaki ndiyo uwekeze. Falsafa hii inawaweka watu kwenye umasikini kwa sababu matumizi huwa hayana mwisho, hivyo hawawekezi. Falsafa ya matajiri ni hii; wekeza kwanza fedha zako, halafu kiasi kinachobaki ndiyo utumie. Falsafa hii inawapa watu utajiri kwa sababu wanawekeza kwa kila kipato wanachoingiza.
18. Unahitaji vitu vitatu katika kufanikiwa, kwanza ujuzi ambao unakuwezesha kuwasaidia wengine. Mbili; unahitaji kuwa na bidhaa au huduma ambayo unawauzia watu hao unaotaka kuwasaidia. Tatu unahitaji kuwa na timu bora ya watu wa kukusaidia, kwa sababu huwezi kufanya kila kitu peke yako.
19. Wale unaowaajiri ndiyo wanaokuwezesha kufanikiwa au wanakufanya ushindwe. Ajiri watu wenye uwezo mkubwa, ni vigumu kuwapata, lakini ukiwatafuta utawapata.
20. Njia bora ya kuwahamasisha wale unaowaajiri ni kutambua uwezo na mchango wao na kuwapa zawadi kupitia hatua wanazopiga kwenye kazi zao. Unapotambua mchango wa watu hao na kuwapa zawadi kwa hatua wanazopiga, wanapata msukumo wa kupiga hatua zaidi.

21. Ili kuweza kufanya kazi vizuri na wengine, unapaswa kuwa vizuri kwenye eneo la mawasiliano. Mawasiliano ndiyo yanajenga au kubomoa mahusiano yoyote yale. Ili kufanikiwa, unapaswa kuzingatia maeneo haya matatu muhimu ya mawasiliano; kuelekeza, kufundisha na kuhamasisha. Ukiweza kufanya hayo matatu vizuri, watu watakuwa tayari kufanya kazi na wewe.
22. Jifunze lugha za ziada. Teknolojia inafanya dunia kuwa kijiji, kama huwezi kuwasiliana kwa lugha za mataifa mengine unajiwekea ukomo kwenye mafanikio yako. Licha ya lugha yako mama, unapaswa kujifunza lugha za kimataifa na zenye ushawishi mkubwa. Na kwa zama zetu hizi ni lazima ujue lugha ya KIINGEREZA, halafu sasa kuna lugha nyingine muhimu kujua kama kichina, kispanishi, kifaransa na kiarabu. Hizi ni lugha tano zinazotumiwa na watu wengi duniani, kadiri unavyojua lugha nyingi katika hizo ndivyo unavyokuwa na wigo mpana.
23. Msingi mwingine wa Jim Rhon katika falsafa yake hii ni huu; FAIDA NI BORA KULIKO MSHAHARA. Anasema mshahara utakupa maisha, lakini faida itakupa utajiri. Hivyo hakikisha unafanya kitu ambacho unalipwa kwa faida. Mshahara una ukomo, lakini faida haina ukomo. Kama umeajiriwa hakikisha unaanza biashara ya pembeni ambayo itakuingizia faida, na siyo kuwa na kazi ya pembeni ambayo inakupa mshahara, unazidi kujiwekea ukomo.
24. Kuwa makini na fursa mpya ambazo zinaahidi mafanikio makubwa bila ya kazi. Jim anasema njia ya kuelekea kwenye utajiri haijabadilika kwa miaka elfu moja iliyopita na haitabadilika kwa miaka mingi ijayo, lazima utoe thamani kwa wengine. Kama fursa inaahidi kupata utajiri ukiwa umelala, kimbia haraka, unataka kutapeliwa.
25. Ili kuepuka kutapeliwa kwa fursa usizoelewa usahihi wake, jiwekee msingi ambao utakuwa unaufuata katika kufanya maamuzi inapokuja kwenye fursa. Chagua mambo na maeneo gani utakayojihusisha nayo na yapi ambayo utayaepuka kabisa. Msingi huu siyo tu utakuepusha na kutapeliwa, bali pia utakulindia muda wako usiupoteze kwa kukimbizana na kila aina ya fursa.
26. Falsafa yako ya mafanikio siyo msaafu ambao haubadiliki, bali utaendelea kuiboresha kadiri unavyokwenda. Utaboresha falsafa hiyo kupitia uzoefu wako binafsi, kwa hatua unazochukua na matokeo unayopata. Lakini pia utaiboresha kwa kujifunza kupitia wengine, angalia makosa wanayofanya wengine na usiyarudie kwenye maisha yako.

27. Pia jijengee mtazamo sahihi kuhusu maisha yako na mafanikio, huu utaiwezesha falsafa yako kuwa hamasa kwako kufanikiwa. Andika malengo yako makubwa mara kwa mara na jijengee taswira ya malengo hayo na hilo litakusukuma zaidi.
28. Kumbuka huwezi kukwepa kazi, falsafa unayokuwa nayo ni mwongozo, haitaleta mafanikio yenyewe. Lazima uweke kazi sana ili kufanikiwa. Huwezi kukwepa kazi, tena hasa na siyo ya kitoto, katika safari yako ya mafanikio.
29. Ili kufikia uhuru wa kifedha unapaswa kuzingatia vitu viwili muhimu sana, moja ni kuwa na njia ya uhakika ya kuingiza kipato, ambayo inakua kadiri unavyoweka juhudi na mbili ni kuepuka sana mikopo, usiingie kwenye madeni yoyote yale. Ukizingatia vitu hivi viwili, mafanikio na utajiri kwako ni swala la muda tu.
30. Hatua sita za kuelekea kwenye maisha ya mafanikio makubwa;
    Moja; kuwa na uzalishaji, fanya kazi.
    Mbili; thamini mahusiano muhimu kwenye maisha yako.
    Tatu; heshimu asili yako, tamaduni na historia ya chimbuko lako.
    Nne; jali afya yako ya kiroho, jijenge vizuri kiimani.
    Tano; boresha mahusiano yako ya karibu, yale mahusiano muhimu zaidi kwenye maisha yako.
    Sita; panda mbegu, kazi yako kwenye maisha ni kupanda mbegu, na kisha asili itauwezesha mti kutokea. Maana yake wewe anzisha na asili itakupa nguvu ya kuendelea.

Rafiki, hii ndiyo falsafa ya maisha ya mafanikio kutoka kwa Jim Rhon, tuweke mafunzo haya kwenye maisha yetu na hatutabaki pale tulipo sasa.

Uchambuzi huu wa kitabu umeandaliwa na Dr. Makirita Amani.

Dr Makirita ni daktari wa binadamu, kocha wa mafanikio, mwandishi na mjasiriamali. Kuendelea kupata chambuzi hizi za vitabu kwenye TANO ZA JUMA, hakikisha unajiunga na channel ya TANO ZA JUMA ambayo ipo kwenye mtandao wa telegram.

Kujiunga ni bure kwa juma la kwanza, kisha baada ya hapo unachagua kulipa tsh elfu moja kwa juma, au elfu tatu kwa mwezi au elfu 30 kwa mwaka. Kwa maelezo zaidi tuma ujumbe kwenda namba 0717396253, ujumbe utumwe kwa njia ya telegram pekee.

Karibu sana.